

Demokrasia yajidhihirisha uchaguzi wa wajumbe bodi ya MJUMITA

Na. Rahima Njaidi, Mkurugenzi - MJUMITA

Katika hali ambayo wanachama wengi wa MJUMITA walivutiwa nayo ni namna ambazo demokrasia ilivyochukua mkondo wake katika uchaguzi wa viongozi wa bodi katika mkutano mkuu wa mwaka wa MJUMITA uliofanyika mwezi wa 11 mwaka 2011.

Katika uchaguzi huo wanachama wengi walijitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wa bodi ya MJUMITA tofauti na chaguzi za miaka ya nyuma. Kila mwanachama alipewa dakika 5 kuelezea sera zake na baadae uchaguzi ulifanyika. Hata hivyo, pamoja na kujitokeza kwa wanachama wengi kuwania nafasi hizo za uchaguzi, wajumbe wa bodi ambao walikuwa wamemaliza muda wao na hivyo kuomba tena fursa ya kuendelea kuongoza bodi hiyo ndio waliochaguliwa katika uchaguzi huo. Wajumbe wa bodi waliochanguliwa na nyadhifa zao ni kama ifuatavyo;

Mwenyekiti	Makamu Mwenyekiti
REVOCATUS NJAU	LENETH MOTO
Mjumbe Kanda ya Mashariki	Mjumbe kanda ya Magharibi
JULIANA JOHN MWENDA	EMMANUEL KARAYENGA
Mjumbe kanda ya Kusini	Mjumbe Nyanja za juu kusini
ATHUMANI MTIMBWA	DOMINIC VENANCE KOMBA
Mjumbe kanda ya Kati	
KWANTLEMA KHWANTLAY	

Kwa heshima kubwa napenda kuwapongeza wanachama wote waliojitokeza kuwania nafasi mbali mbali wakati wa uchaguzi. Aidha kwa namna ya kipekee kabisa nawapongeza wajumbe wote wa bodi waliochaguliwa na nawatakia kheri katika utumishi wao katika bodi ya MJUMITA.

Baadhi ya wajumbe na viongozi walioudhuria mkutano kutoka kulia ni ndg. Dominic Venance Komba (mjumbe kanda nyanda za juu kusini), Emmanuel Karayenga (mjumbe kanda Magharibi), Leneth Moto (Makamu mwenyekiti), Revocatus Njau (Mwenyekiti), Juliana J. Mwenda (Mjumbe kanda ya Mashariki), Kwantlema Khwantlay (Mjumbe kanda ya Kati), Athmani Mtimbwa (Mjumbe Kanda ya kusini)

